TANGAZO LA SERIKALI NA. 209 la tarehe 22/3/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 8(1) na 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA UENDESHAJI WA MASOKO NA MAGULIO YA HALMASHAURI YA MJI MAFINGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Uendeshaji wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Mji Mafinga ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Mji Mafinga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"dalali" maana yake ni mtu yeyote anayeuza bidhaa za sokoni kwa njia ya mnada kwa niaba ya mwenye bidhaa kwa mujibu wa sheria na taratibu za soko;

"gulio" maana yake ni soko la wazi linalofanyika kwa wakati maalumu kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji Mafinga;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu Sheria Ndogo hii;

"kodi ya pango" maana yake ni kodi inayolipwa na mpangaji kwa Halmashauri kila mwezi au kila siku kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"makasha" maana yake ni vifaa maalumu vya kubebea, kufungashia au kuhifadhia bidhaa au mazao na inajumuisha matenga, viroba, magunia, karatasi ngumu, maboksi, masanduku ya mbao na mengine vyenye asili hiyo;

"meza au kizimba" maana yake ni kitu au kifaa kinachotumika kuweka bidhaa kwa ajili ya kuuza sokoni au gulioni;

"mfanyabiashara" maana yake ni mtu yeyote anayeuza bidhaa sokoni au gulioni kwa jumla au rejareja;

"meneja wa soko" maana yake ni mtu yeyote aliyeteuliwa au aliyeajiriwa na Halmashauri kusimamia shughuli zote katika soko;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga pamoja na afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada" maana yake ni soko la wazi ambalo mali au vitu mbalimbali vinauzwa kwa ushindani wa bei kwa kauli na kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"mnunuzi" maana yake ni mtu yoyote anayenunua bidhaa au mazao sokoni au katika eneo la mamlaka ya Halmashauri;

"mpangaji" maana yake ni mtu anayetumia kwa namna yoyote ile kibanda, chumba, meza au kizimba kinachomilikiwa au kilichojengwa kwenye ardhi ya Halmashauri;

"muuzaji" maana yake ni mtu yoyote anayeuza bidhaa au mazao katika soko au eneo lililoidhinishwa na Halmashauri;

"soko" maana yake ni eneo maalumu la biashara lililotengwa na Halmashauri kwa matumizi ya kuuzia au kununulia bidhaa na inajumuisha gulio;

"wakala" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Halmashauri kutekeleza majukumu chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri;

"wadau wa soko" maana yake ni wafanyabiashara binafsi, vikundi vilivyoandikishwa katika kamati ya wadau wa soko au gulio na kuwasilishwa kwa mkuu wa soko, au vyama vya ushirika vinavyofanya shughuli za biashara katika soko;

"ushuru" maana yake ni kiasi cha fedha kinachotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"vikundi" maana yake ni vikundi vya ushirika vya wafanyabiashara au umoja wa vikundi vya wafanyabiashara vilivyosajiliwa au kuandikishwa na kuwasilishwa katika kamati ya soko au gulio na kwa mkuu wa soko na kutambuliwa na Halmashauri; na

"mazao" maana yake ni mavuno ya shambani au maliasili yanayoingizwa kwenye soko au ndani ya eneo la mamlaka ya Halmashauri.

Mamlaka na majukumu ya Halmashauri juu masoko, magulio na minada

4. Halmashauri itakuwa na mamlaka na kutekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kuanzisha, kusimamia na kuendesha masoko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) kuendeleza masoko;
(c) kusimamia usafi na usalama wa masoko na magulio;
(d) kusimamia ufikishaji wa huduma za kijamii katika soko na gulio;
(e) kugawa na kupangisha soko kwa vyumba, meza au vizimba;
(f) kutenga maeneo kwa ajili ya magulio; na
(g) kusajili wafanyabiashara wote katika masoko yote ya Halmashauri.

Meneja wa soko

5.-(1) Kutakuwa na meneja wa soko atakayeteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kusimamia shughuli za uendelezaji wa masoko.

(2) Bila kujali aya ya (1), meneja wa soko atakua na majukumu yafuatayo:

(a) kusimamia ukusanyaji wa ushuru na ada mbalimbali;

(b) kusimamia usajili wa wadau wa soko kwa kushirikiana na kamati ya wadau wa soko;

(c) kuimarisha huduma za ulinzi, maji na umeme katika masoko;

(d) kusimamia usafi na uondoshaji wa taka katika soko;

(e) kuhakikisha kuwa bidhaa haziuzwi kwenye eneo ambalo haliruhusiwi kwa shughuli hiyo;

(f) kuzuia ujenzi holela katika soko; na

(g) kutekeleza majukumu mengine yoyote yatakayoagizwa na Halmashauri.

(3) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kuajiri wakala ambaye atawajibika kusimamia uendeshaji wa soko kwa niaba yake.

(4) Wakala atakayeteuliwa chini ya aya ndogo ya (2) atasimamia shughuli za uendeshaji wa soko kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ndogo ya (2) na masharti ya mkataba wa uwakala kati yake na Halmashauri.

Kamati ya wadau wa soko

6.-(1) Kutakuwa na kamati ya wadau wa soko ambayo itaundwa na wadau wa soko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Kila kikundi cha ushirika katika soko kitakuwa na mwakilishi mmoja katika kamati ya wadau wa soko.

(3) Kamati ya wadau wa soko itatakiwa kuweka

utaratibu maalumu wa kuwapata viongozi wake, kuwaondoa madarakani na uendeshaji wa shughuli zake na kuuwasilisha kwa Halmashauri.

(4) Vikao vya kamati ya wadau wa soko vitafanyika mara moja kila mwezi.

(5) Meneja wa soko atakuwa katibu katika vikao vyote vya kamati ya wadau wa soko.

(6) Muda wa wajumbe wa kamati ya soko kuwa madarakani ni miaka mitatu.

Majukumu ya kamati

7. Kamati ya wadau wa soko itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuhakiki biashara zinazoendeshwa katika soko;
(b) kuboresha ustawi wa wadau wa soko;
(c) kuhakikisha uwepo wa nidhamu katika shughuli za soko;
(d) kuhakikisha wadau wote wa soko na gulio wanalipa ushuru na ada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(e) kukuza na kuendeleza mfumo wa biashara;
(f) kuhakikisha kila eneo la mdau na soko kwa ujumla linakuwa safi muda wote;
(g) kutekeleza kazi nyingine watakazoelekezwa na Meneja wa soko kulingana na Sheria ndogo hii; na
(h) kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwepo sokoni.

Kamati ndogo

8.-(1) Kamati ya wadau wa soko itaunda kamati ndogo zenye wajumbe wanne kutoka miongoni mwa wajumbe wa kamati ya wadau wa soko ambazo ni-

(a) kamati ndogo ya miundombinu na usafi;
(b) kamati ndogo ya utawala na biashara; na

(c) kamati ndogo ya ulinzi na usalama.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), kamati ya wadau wa soko inaweza kuunda kamati ndogo yoyote kwa kadri itakavyoona inafaa.

Usajili wa wadau

9. Mtu anayetaka kufanya biashara katika eneo la soko atajisajili kwa meneja wa soko na meneja akishirikiana na kamati ya wadau wa soko kwa lengo la kumtambua na kumworodhesha katika rejesta ya wadau wa soko.

Wajibu wa mfanyabishara

10. Mfanyabiashara katika eneo la soko atakuwa na wajibu wa-

(a) kujisajili katika rejesta ya wadau wa soko;
(b) kulinda na kuhifadhi miundombinu ya soko;
(c) kufanya biashara katika maeneo yanayoruhusiwa;
(d) kufanya usafi katika eneo lake la biashara;
(e) kulipa ushuru na ada kwa wakati;
(f) kutobandika au kutobandua tangazo bila idhini ya meneja wa soko;
(g) kutotumia lugha ya matusi, kuudhi au kashfa katika eneo la soko;
(h) kushiriki usafi wa jumla wa soko;
(i) kutoweka bendera ya chama chochote cha siasa ndani ya eneo la soko;
(j) kutofanya shughuli za kisiasa katika eneo la soko;
(k) kutotupa taka ovyo au kutiririsha maji machafu;
(l) kutowasha moto maeneo yasiyohusika ndani ya soko; na
(m) kuheshimu masharti ya upangaji aliyopewa na Halmashauri na maelekezo atakayopewa na Halmashauri, meneja wa soko na kamati ya wadau wa soko.

Muda wa

11.-(1) Soko litakuwa wazi siku zote kuanzia saa

biashara

kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Meneja wa soko, kwa kushauriana na Mkurugenzi, anaweza kufunga soko kwa ajili ya matengenezo au sababu nyingine yoyote ya dharura pale itakapoonekana inafaa.

(3) Isipokuwa kwa sababu nyingine za dharura, meneja wa soko hatakuwa na mamlaka ya kufunga soko kwa sababu za matengenezo isipokuwa tu baada ya kutoa notisi ya siku saba kwa wadau wa soko kuhusu kusudio la kufunga soko kwa ajili ya matengenezo.

Ushuru wa soko mnada au gulio

12. Halmashauri itatoza ushuru wa soko kutoka kwa kila mfanyabiashara aliyesajiliwa kufanya biashara katika eneo la soko kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Kodi ya pango

13.-(1) Mfanyabishara katika soko atalipa kodi ya pango kwa kizimba au kibanda kwa mujibu wa mkataba wa upangishwaji.

(2) Wafanyabiashara katika soko ambao hawana mkataba watalipa kodi ya pango kwa kizimba au kibanda kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(3) Halmashauri inaweza, kwa makubaliano maalumu, kumruhusu mtu yeyote kujenga banda la biashara katika eneo la soko au kufanya ukarabati au marekebisho ya chumba, kibanda, meza au kizimba.

Usimamizi wa magari

14.-(1) Magari yote yanayotumika kufikisha mazao au bidhaa sokoni yatashusha bidhaa katika maeneo yaliyoainishwa kwa ajili hiyo.

(2) Meneja wa soko anaweza kuamua na kusimamia idadi ya magari yatakayoruhusiwa kushusha bidhaa au mazao sokoni.

(3) Meneja wa soko, kwa kadiri atakavyoona inafaa, anaweza kuondoa gari au kuzuia gari kuingia katika sehemu iliyotengwa.

Kibali cha minada na magulio

15. (1) Mtu anayekusudia kuendesha minada ya mazao, nguo na bidhaa nyingine katika masoko ataomba kwa Halmashauri kibali maalumu kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Halmashauri inaweza kutoa kibali maalumu cha kufanyika kwa magulio katika maeneo yatakayoteuliwa na Halmashauri kwa madhumuni hayo.

Usafi wa soko

16.-(1) Mfanyabiashara anayefanya biashara katika eneo la soko atawajibika kuweka eneo lake katika hali ya usafi wakati wote pamoja na kuzingatia kanuni za afya.

(2) Meneja wa soko kwa kushirikiana na kamati ya wadau wa soko atasimamia usafi wa jumla wa soko kila siku ya jumamosi ya mwisho wa mwezi.

Mifugo kutoingizwa sokoni

17. Mtu yeyote hataingiza mifugo sehemu yoyote ndani ya soko, magulio au minada, isipokuwa sehemu maalumu iliyoteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya mifugo.

Ufungaji wa bidhaa ziletwazo sokoni au gulioni

18.-(1) Bidhaa zote ziletwazo sokoni au gulioni zitawekwa katika makasha maalumu ya kusafirishia bidhaa.

(2) Endapo bidhaa imefungwa kwa kutumia majani wakati wa kusafirisha, majani hayo yatabaki ndani ya chombo kilichotumika kusafirisha bidhaa hiyo na mwenye bidhaa au msafirishaji atawajibika kuhakikisha majani hayo yanasafirishwa na kutupwa katika dampo la Halmashauri soko kwa gharama zake.

Makosa

19. Mtu anatenda kosa iwapo mtu huyo-

(a) anabandika au kubandua tangazo lolote katika eneo la soko bila idhini ya meneja wa soko au afisa mwidhiniwa;

(b) anauza pombe ndani ya soko, gulio au mnada bila leseni ya vileo iliyotolewa na Halmashauri;

(c) anafanya shughuli yoyote inayohusisha matumizi ya moto isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya Halmashauri;
(d) anatembeza bidhaa ndani ya soko bila kibali cha Halmashauri;
(e) anaweka bendera ya chama chochote cha siasa ndani ya eneo la soko au gulio;
(f) anafanya shughuli za siasa ndani ya soko au gulio;
(g) anaharibu miundombinu ya soko au gulio;
(h) anafanya ujenzi au ukarabati bila kibali;
(i) anatumia lugha ya matusi, kufanya vurugu au ugomvi ndani ya soko;
(j) anafanya shughuli yeyote kwenye eneo ambalo haliruhusiwi au halijatengwa kwa ajili ya shughuli hiyo;
(k) anatupa taka au kutiririsha maji machafu katika eneo lisiloruhusiwa;
(l) anawasha moto maeneo yasiyoruhusiwa;
(m) anatumia kama stoo au matumizi mengine kinyume na masharti ya katika mkataba au leseni;
(n) anaendelea na biashara baada ya muda wa biashara ulioainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Adhabu

20. Mtu anayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Ufifilishaji makosa

21. Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kulipa kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi katika fomu maalumu iliyoainishwa katika

Jedwali la Tatu la na kuwa tayari kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 12 na 13)*

USHURU NA KODI YA PANGO KATIKA MASOKO MINADA NA MAGULIO

(i) Ushuru wa Soko

| Namba | Aina ya bidhaa | Kiwango cha na ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 1,000 @ gunia la kilo 90 |
| 2. | Maharage | 1,000 @ gunia la kilo 90 |
| 3. | Mpunga | 1,000 @ gunia la kilo 75 |
| 4. | Dagaa | 1,000 @ gunia la kilo 70 |
| 6. | Samaki | 1,000 @ tenga kilo 50 |
| 10. | Vitunguu | 1,000 @ gunia la kilo 70 |
| 11. | Alizeti | 500 @ gunia la kilo 40 |
| 12. | Kabeji, Machungwa, Miwa, Nanasi, Ndizi, Parachichi | 5000 kwa tani moja,<br>500 kwa mkungu wa ndizi<br>1,000 kwa tenga la kilo 50 |
| 13. | Viazi | 1,000 @ gunia la kilo 100 |
| 14. | Hoho | 500 kwa tenga kilo 50 |
| 15. | Karanga | 2,000 @ gunia la kilo 90 |
| 16. | Njegere maganda | 1,000 @ gunia la kilo 90 |
| 17. | Nyanya | 1,000 @ tenga la kilo 50 |
| 18. | Mchele | 1,000 @ gunia la kilo 100 |
| 19. | Unga | 500 @ gunia la kilo 80 |
| 20 | Bidhaa nyingine ambayo haijatajwa | 1,000 @ tenga/gunia |

(ii). Ushuru wa minada na magulio

| Namba | Aina ya Bidhaa | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng’ombe | 5,000 @ ngombe |
| 2. | Kondoo | 1,000 @ kondoo |
| 3. | Mbuzi | 1,000 @ mbuzi |
| 4. | Bidhaa zinazotengenezwa viwandani/ karakana | 500 @ siku |
| 5. | Wauza mitumba | 500 @ siku |
| 6. | Wauza bia na vinywaji baridi | 1,000 @ siku |
| 7. | Wauza nafaka | 500 @ gunia |

*Tangazo La Serikali Na. 207 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Ndege (kuku, bata) | 500 @ siku |
| 9. | Pombe za asili | 500 @ siku |
| 8. | Wauza madawa ya asili | 500 @ siku |
| 9. | Wauza vipuri vya baiskeli,pikipiki,magari | 500 @ siku |
| 10. | Wauza dagaa | 500 @ siku |
| 11. | Wauza samaki | 500 @ siku |
| 12. | Wauza chumvi, nyama na mboga za majani | 500 @ siku |
| 13. | Wauza vyungu | 500 @ siku |
| 14. | Wauza vyombo vya nyumbani | 500 @ siku |
| 15. | Wauza viatu | 500 @ siku |
| 16. | Wauza nguo mpya | 500 @ siku |
| 17. | Mafundi baiskeli | 500 @ siku |
| 18. | Bidhaa nyingine ambazo hazijatajwa | 500 @ siku |
| 19. | Mifugo mingine ambayo haijatajwa | 500 @ siku |
| 20. | Ng'ombe waliopelekwa na kuingizwa mnadani lakini hawajauzwa | 1000 @ Ng'ombe |

(iii). Kodi ya Pango ya eneo, vibanda au vizimba vya biashara kwa wafanyabiashara wasio na mikataba ya upangaji katika eneo la soko kuu Mafinga

| Namba. | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ada kwa mwezi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Vizimba | 9,000 |
| 2. | Matundu ya kuku | 15,000 |
| 3. | Mama/baba lishe | 20,000 |
| 4. | Vioski/mabanda ya mitumba/bucha | 50,000 |
| 5. | Maduka | 100,000 |
| 6. | Stoo | 200,000 |

(iv). Viwango vya kodi za pango la vyumba, vibanda vya biashara kwa mwezi maeneo mengine kwa wasio na mikataba

| Namba. | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|

*Tangazo La Serikali Na. 207 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Vizimba | 6,000 |
| 2. | Mama /baba lishe | 10,000 |
| 3. | Vioski/Mabanda ya Mitumba na Bucha | 10,000 |
| 4. | Maduka | 25,000 |
| 5. | Stoo | 30,000 |

(v). Ushuru wa kupakia na kushusha mizigo katika masoko

| Namba. | Aina ya chombo cha usafiri | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari au bajaji 500 kgs | 500 |
| 2. | Gari tani 1 pick up | 1,000 |
| 3. | Gari tani 1.5 | 1,500 |
| 4. | Gari tani 2 | 2,000 |
| 5. | Gari tani 3 | 3,000 |
| 6. | Gari tani 4 | 4,000 |
| 7. | Gari tani 5 | 5,000 |

(vi) Ushuru katika soko la mbao/mazao ya misitu

| Namba | Aina ya Zao la Misitu | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mbao | 100/= kwa ubao mmoja |
| 2. | Mirunda | 50/= kwa mrunda |
| 3. | Nguzo za simu | 500/= kwa nguzo |
| 4. | Nguzo za umeme | 1,000/= kwa nguzo |
| 5. | Kuni | 3,000/=kwa tani moja |
| 6. | Mkaa | 1,000/= kwa gunia la kilo 50 |
| 7. | Mabanzi | 50/= kwa banzi |
| 8. | Mazao mengine ya misitu | 5,000/= kwa tani moja |

## JEDWALI LA PILI

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 15(1)(2))*

### KIBALI CHA KUTUMIA SOKO

1. Jina la Mwombaji ……………………………………………..
2. Anuani ya mwombaji ……………………………………………
3. Kibali cha ……………………………………………………..
4. Eneo ambalo kibali hicho kitatumika ……………………………...
5. Muda wa kibali ni kuanzia tarehe……………hadi tarehe…………
6. Masharti ya kutumia kibali hicho…………………………………………..
   a) ………………………………………………
   b) ………………………………………………
   c) ………………………………………………
   d) ………………………………………………
   e) ………………………………………………
7. Nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa ni kweli tupu na niko tayari kuzingatia masharti ya kibali endapo nitapewa kibali hicho.
   Jina la Mwombaji …………………………………
   Saini ………………………………………………
   Tarehe …………………………………………..
8. Kibali hiki hakihamishiki

KWA MATUMIZI YA OFISI TU
Namba ya kibali……………. Tarehe………………………. Mahali …………….
Stakabadhi Na.………………………ya Tarehe………………………….

Jina la afisa muidhinishaji………………………………….
Saini……………………cheo………………………….
Muhuri

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 21)*

### FOMU YA KUFIFILISHA MAKOSA

Mimi,……………………………………………………. nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya……………………………………..…….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Mafinga, kwamba mnamo tarehe;…… ya Mwezi;….….

*Tangazo La Serikali Na. 207 (Linaendelea)*

Mwaka;…….… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya Uendeshaji wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Mji Mafinga ya Mwaka 2024.
Nipo tayari kutimiza wajibu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hiyo.

Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.
Leo tarehe…....... ya Mwezi………… Mwaka…………..
Jina:………………………………..…………………….
Saini:………………………..……………………………

MBELE YANGU:
Jina:…………………………..……..……………………
Wadhifa:……………………………………………...…….
Saini:……………………………………………………………
Tarehe:………………………………………………………….

*Tangazo La Serikali Na. 207 (Linaendelea)*

Lakari ya Halmashauri ya Mji Mafinga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Mafinga uliofanyika Tarehe 14 mwezi 02 Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya ;-

AYUBU J. KAMBI
*Mkurugenzi*

REGNANT Z. KIVINGE

*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji Mafinga*

NAKUBALI

/

L.S

DODOMA
31 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa)*